biovision

# Mkulima Mbunifu

Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki

Toleo la 112 | Januari 2022

## Yaliyomo

Kanuni za kilimo hai na mazingira 2
Samadi itokanayo na kinyesi cha Popo 5



Umuhimu wa mzani na ufugaji wa Nguruwe 6
Lishe bora husaidia ukuaji wa mtoto 7

# Umejiandaa vipi na safari mpya 2022

***Kila mwaka unapoanza wakulima na wafugaji pia tunakuwa tunaanza safari mpya katika uzalishaji. Kwa mantki hiyo basi, ni muhimu kufahamu kuwa safari yako ya uzalishaji inaanzia wapi, unaelekea wapi, nini kusudio la safari yako, na matokeo unayotarajia.***

Ni muhimu sana kwako Mkulima na mfugaji kuhakikisha kuwa, umeweka mipango thabiti na mikakati ya kufikia malengo yako uliyojiwekea.

Ni vyema kujiuliza kuwa, kama sijajiwekea malengo na mikakati mipya je, itakuwaje. Endapo hadi sasa haujapanga yale unayokusudia kufanya katika mwaka huu wa 2022, basi hakikisha kwa muda uliosalia unakaa chini na kuweka mikakati yako sawa katika utaratibu ambao utakufanya uweze kufanya yote kwa ufanisi na hatimae kufikia mwisho mzuri wenye mafanikio.

Njia nzuri ni kuandaa orodha, na kuweka vipaumbele hatua kwa hatua kwa kila jambo unalokusudia kufanya kwenye shughuli zako kwa mwaka huu.




## Mpendwa Mkulima

*Heri ya mwaka mpya wa 2022 msomaji wa Jarida la Mkulima Mbunifu. Ni matumaini yetu kuwa mwaka umeanza salama kabisa, na hatuna budi kukupa hongera pia kwa kuanza mwaka huu ukiwa mzima. Vinginevyo basi yote ni kushukuru tu.*

*Pamoja na hayo yote, ni imani yetu kuwa mikakati uliyoiweka kwa ajili ya kufunga na kufungua mwaka hakika imeanza kutekelezwa barabara.*

*Endapo haukuweza kuweka mipango thabiti kuwa ni kipi utaanza kutekeleza kwa mwaka huu, basi ni vyema sasa ukaweka mipango hiyo na kuitekeleza kwa kuwa muda hautakungoja usipojipanga vizuri.*

*Kuna msemo usemao, ukipanga kwa uthabiti, umepanga kufanikiwa na ukipanga ovyo ovyo, basi umepanga kufeli. Hivyo hakikisha unakuwa na mipango thabiti itakayokuwezesha kufikia malengo yako.*

*Pamoja na kujipanga, ni muhimu sana kutafuta na kupata elimu sahihi itakayokusaidia katika shughuli zote ambazo umepanga kutekeleza kwa mwaka mzima.*

*Endapo unahitaji kuzalisha mazao kwa ajili ya chakula cha familia na biashara, basi tafuta kupata taarifa na elimu sahihi juu ya zao husika. Hii ni pamoja ufahamu wa mbegu bora, namna ya kupanda, matunzo na namna ya kukabiliana na wadudu na magonjwa endapo yatajitokeza.*

*Sambamba na mazao, fanya vivyo hivyo kwa uzalishaji wa mifugo ya aina mbalimbali, miti na uzalishaji wa matunda, na inapofikia msimu wa kuvuna na kuuza, usikurupuke.*

Kwa uhitaji wa jarida hili kila mwezi wasiliana nasi kwa kutupigia simu au kwa anwani kwa kupitia barua pepe, facebook, tovuti na sanduku la posta kama zilivyoonyeshwa hapa;

+255 717 266 007
http://www.facebook.com/mkulimambunifu
http://twitter.com/mkulimambunifu
mkulimambunifu.org
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org

Wasiliana na *MkM*,
S. L. P 14402, Arusha,
Simu:
0717 266 007, 0762 333 876,
Barua pepe:
info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org

Mkulima Mbunifu

# Kanuni za kilimo hai zinavyofungamana na mazingira

***Kanuni ndio msingi wa kilimo hai na mchango unaoweza kuifanya dunia kuboresha kilimo duniani kwa ujumla. Kilimo ni moja ya shughuli muhimu zinazofanywa na binadamu kwa ajili ya kupata mahitaji ya kila siku ili kujikimu. Historia, mila na tamaduni za watu katika jamii zinaambatana na maendeleo katika kilimo.***



Mboga mboga zikizalishwa kwa misingi ya kilimo hai na katika mazingira safi hupelekea mazao bora

**Ayubu Nnko**

Kanuni zinazotumika katika kilimo kwa ujumla zinahusisha mtazamo wa watu juu ya udongo, maji, mimea na wanyama katika kuzalisha, kuandaa na kusambaza chakula na bidhaa nyinginezo.

Kanuni hizo zinaonesha namna watu wanavyo ona uhai na mandhari ya ardhi, mahusiano miongoni mwao na mwelekeo wa matumaini kuhusu vizazi vijavyo. Kanuni za kilimo hai zinalenga kuhusisha vuguvugu la kilimo hicho katika nyanja zote, kutoa mwongozo katika kuweka vipaumbele juu ya maendeleo, mipango na viwango. Isitoshe, kanuni hizi zinawakilisha mtazamo wake kidunia.

**Kanuni za msingi za kilimo hai:** Kuna kanuni nne za msingi za kilimo hai.

I. Kanuni ya Mazingira
II. Kanuni ya Afya
III. Kanuni ya Haki na Usawa
IV. Kanuni ya Huduma

Kanuni hizi zimefungamana na kwa ujumla wake zinabeba kivitendo matarajio ya kilimo hai japo kila kanuni ina maelezo yake na dhana iliyobebwa ndani yake huku zikizingatia afya ya mazingira na mimea, wanyama na binadamu.

## Kanuni ya mazingira

Kilimo hai sharti kisimamie na kujali uhai wa mfumo wa mazingira na mzunguko asilia, kuishi na kufanya kazi sanjari na kuchangia katika kufanya kilimo kiwe endelevu.

Kanuni hii huweka msingi wa kilimo hai katika kuhusisha na kuhifadhi mazingira. Inasisitiza juu ya uzalishaji unaoyajali na kutegemea mchakato endelevu wa kimazingira.

Hali iliyobora na ustawi hupatikana kwa kutegemea mazingira ya uzalishaji unaojali uhai wa viumbe wengine. Kwa mfano uzalishaji wa mazao unapaswa kuzingatia uhai wa udongo; ufugaji wa wanyama unaozingatia mfumo wa kimazingira.

Pamoja na kuwa kilimo hai kinaendana na mazingira ya kawaida na tamaduni za mahali popote duniani kwa kuzingatia kanuni za msingi, matumizi ya pembejeo sanisia/kemikali ni sharti yasiwepo, kuongeza uwajibikaji katika kutumia rasilimali na maliasili, pale inapowezekana kurejeshwa upya na kutumika tena. Kuwa na usimamizi sahihi wa malighafi na nishati ili kuboresha mazingira na kuhifadhi maliasili na rasilimali.

Kilimo hai lazima kifanikishe uwiano wa kimazingira kwa kubuni na kuhimiza mfumo wa uzalishaji unaoweka mazingira bora kwa makazi na kutunza urithi wa kimaumbile na kilimo.

Wanaozalisha, kusindika, kuuza au kusambaza bidhaa za kilimo hai wanawajibika kulinda uwiano huu kwa manufaa ya mazingira kwa ujumla ikiwa ni pamoja na hali ya hewa, viumbe, bayoanuai, hewa na maji.

## Kanuni ya Afya

Kilimo hai sharti kiwe endelevu na kudumisha rutuba ya udongo, kiboreshe afya ya mimea, wanyama, binadamu katika sayari hii kama kitu kimoja. Kanuni hii inaashiria kuwa afya ya watu au jamii haiwezi kamwe kutengwa na afya ya kimazingira-ardhi yenye afya huzalisha mazao yenye ubora kwa afya na uhai wa binadamu na wanyama.

Afya ni mfumo wa uhai na taratibu za maisha ikimaanisha kutokuwepo magonjwa, kujali na kutunza mwili, akili, ustawi wa jamii, mazingira bora na mazuri kuishi. Uwezo wa kujikinga, kushiriki katika uumbaji na kujijali na tabia ya msingi na muhimu kwa afya bora, jukumu la kilimo hai liwe katika ulimaji, usindikaji, usambazaji.

Usambazaji au ulaji ni kuendeleza na uboresha afya na uhai, mfumo wa mazingira na viumbe aina zote kuanzia kwenye udongo hadi binadamu.

Kwa hakika, kilimo hai kinalenga katika uzalishaji wa chakula kinachokidhi viwango vya ubora na usalama wa hali ya juu ili kuchangia katika kujikinga na kujenga siha nzuri.

Kwa kuzingatia afya, usalama na uhai, kanuni za kilimo hai zinazuia matumizi holela ya mbolea, madawa ya wadudu au magonjwa ya mifugo na viatilifu au vinasaba vinavyoongezwa katika hifadhi ya vyakula ambavyo vinaweza kusababisha madhara ya kiafya kwa mlaji au mtumiaji.

Itaendelea toleo lijalo. »»

*Mkulima Mbunifu* ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa kila mwezi na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation

African Insect Science for Food and Health

**Wachapishaji:** African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

**Mpangilio**: Cathbert Msemo 0652 731 123
**Mhariri:** Erica Rugabandana
**Mhariri Msaidizi:** Flora Laanyuni
**Anuani:** *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)
S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366
Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876
Barua pepe: info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org

# Ekari moja ya ardhi iliyopangiliwa huimarisha uchumi wa familia

***Watu wengi hudhani matumizi bora ya ardhi ni kujenga nyumba kubwa ya kisasa na kuweka sakafu ya matofali madogo (pavement) bila kujali ukubwa wa eneo hilo. La hasha! Matumizi bora ya ardhi ni kuwa na eneo kubwa ama dogo lakini lililopangiliwa vizuri kwa faida ya familia, kiafya na pia kiuchumi.***

**Esther Mbusi**

Ukiwa na eneo ukalipangia vizuri hasa katika uzalishaji utaweza kujipatia mazao ya aina mbalimbali ya mifugo na kilimo kwa ajili ya familia pamoja na kipato kwa kuuza mazao ya ziada kulingana na matumizi ya eneo lako.

Katika makala hii *Mkulima Mbunifu* itakuelekeza ni kwa namna gani unaweza kulitumia eneo la ekari moja kufanya uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo pamoja na kuwa na eneo la kuishi la familia huku ukihakikisha usalama wa chakula kwa familia.




Fanya matumizi bora ya ardhi katika eneo unaloishi, kuboresha afya ya familia na kua na mazingira bora

## Ekari moja ya shamba

Eneo hili la shamba litatumika kufanya kilimo mseto ambacho kitabeba vitu vingi, ikiwemo mazao ya chakula ya aina mbalimbali, mifugo kama vile kuku, ng'ombe, mbuzi lakini pia nyumba ya familia ya kuishi.

Uzalishaji huu pia utakuwa wa gharama nafuu sana lakini wenye faida endapo mkulima atazalisha kwa misingi ya kilimo hai yaani kilimo kinachotumia malighafi za asili bila kuhusisha matumizi ya kemikali za aina yoyote kutoka viwandani.

## Nini cha kufanya

Ili uweze kupangilia eneo hili na kuzalisha kwa tija, ni muhimu kwanza kuamua ni uzalishaji gani unataka kuufanya katika eneo lako yaani kama ni kilimo utahitaji kuzalisha mazao gani, na kwa mifugo utazalisha aina gani ya mifugo kisha kufahamu ni eneo lipi utatumia kuzalisha nini na wapi utajenga nini.

Hii utafanikiwa tu, endapo utachora mchoro namna ambavyo uzalishaji wako utajipanga yaani kama ni nyumba ya kuishi itakaa wapi kama bwawa la samaki na kwanini, kuku au ng'ombe watakaa wapi nk. Kufanya hivi kunasaidia kila unachotaka kuzalisha kiwe mahali panapostahili.

## Namna ya kupanga eneo la ekari moja

Katika eneo la ekari moja, unaweza kupanga uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa kadri unavyopenda lakini pia kwa kuangalia kipi kinafaa wapi. Unaweza kufuata mfano huu;

- Eneo la samaki mita 7 kwa 3 sawa na mita za mraba 21.
- Eneo la kulima mahindi robo eka.
- Rozela robo eka.
- Eneo la migomba mita 15 kwa 5.
- Mita 7 kwa 10 kwa ajili ya mazao ya mizizi kama vile mihogo au magimbi.
- Eneo la kufuga kuku mita 6 kwa 7.
- Eneo la kulima mboga mboga mita 10 kwa 8.
- Mita 10 kwa 6 kwa ajili ya malisho ya mifugo.




Unaweza kujumuisha uzalishaji wa mbogamboga na samaki katika eneo moja

- Mita 8 kwa 7 kwa ajili ya kupanda miti ya kutengeneza dawa za asili.




Eneo la ekari moja ya shamba laweza kutumika kuzalisha mazao na mifugo mbalimbali

## Faida ya kuzalisha mazao haya kwa pamoja

Mkulima anapozalisha mazao haya kwapamoja itamsaidia kupata mahitaji yake ya kifamilia hususani chakula chenye afya kulingana na mazao yaliyopo shambani lakini pia itamsaidia kupata fedha pale ambapo atauza mazao ya ziada ama atazalisha kwa ajili ya biashara.

Uzalishaji wa namna hii utamsaidia mkulima kupunguza gharama za kununua mahitaji ya chakula kutoka sokoni.

***Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na uongozi wa shamba la kilimo hai la St. Joseph Sustainable Organic farm, Mwanga-Kilimanjaro. Simu namba 0626908639***

# Uchafu husababisha magonjwa ya ngozi kwa mifugo

***Wafugaji walio wengi, hudhania kuwa wanyama hawana hadhi ya kufanyiwa usafi au kuwekwa katika mazingira safi kama ilivyo kwa binadamu. Hata kama viwango hutofautiana, lakini ifahamike kuwa mifugo pia inastahili kuishi katika mazingira ambayo ni safi na salama.***

**Method Charles**



Ng'ombe wakitunza kwenye eneo au mazingira machafu huweza kupata magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya ngozi

Mazingira safi husaidia kuepusha wanyama kushambuliwa na magonjwa ya aina mbalimbali yakiwemo magonjwa ya ngozi yanayosababishwa na vimelea vinavyotokana na uchafu.

Moja ya magonjwa ambayo ni hatari sana kwa wanyama yanayotokana na uchafu, ni pamoja na magonjwa ya ngozi na yale yanayosababishwa na minyoo.

Ni jambo la busara sana kuhakikisha kuwa mifugo ipo katika mazingira safi na salama wakati wote

## Fahamu ugonjwa wa ukurutu na namna ya kuudhibiti

Ukurutu ni ugonjwa wa ngozi ambao huambukizwa kwa njia ya kugusana kati ya mnyama aliyeathiriwa na aliye mzima.

Kitaalamu ugonjwa huu hujulikana kwa jina la menji (Mange) na husababishwa na utitiri ambao kitaalamu wanaitwa mange mites.

Wadudu hawa hujikita kwenye ngozi na kufanya ngozi kuwa ngumu kama yenye magaga, humfanya mnyama kuwashwa na mwisho manyoya kupukutika na kuondoka kabisa.

## Aina za ukurutu

Kuna aina nyingi za ukurutu lakini aina kuu nne ndizo zinazojulikana na kushambulia wanyama kwa wingi hapa nchini. Aina hizo ni kama ifuatavyo;

## Ukurutu Demodektiki

Hii ni aina ya ukurutu husababishwa na wadudu ambao hujikita kwenye vijishimo vya vinywelea na matezi na kusababisha kutokea kwa vivimbe ambavyo huwa na muwasho katika sehemu za shingoni, mabegani, usoni, mgongoni. Aidha, husababisha kutokea kwa ute wenye rangi ya kijivu na huweza kuwa na wadudu. Ukurutu huu hushambulia mbwa, ng'ombe, kondoo, mbuzi, farasi, mbwa na nguruwe.

## Ukurutu Sakoptiki

Ukurutu huu huenea kwa njia ya mgusano kati ya mnyama mwenye ugonjwa na asiyekuwa na ugonjwa na huenea kwa haraka sana. Aidha, imebainika kuwa, wanyama wanyonyeshao huambukiza watoto wao haraka sana hasa wakati wa kunyonyesha.

Ngozi ya mnyama mwenye sakoptiki huwa ngumu, huvimba na huwa na muwasho.

## Ukurutu Soroptiki

Aina hii ya ukurutu hushambulia ng'ombe, mbuzi, kondoo, farasi, nguruwe, mbwa na paka. Ugonjwa huu huenezwa kwa njia ya kugusana kati ya mnyama aliyeathirika na yule ambaye hajaathirika.

## Ukurutu korioptiki

Hii ni aina nyingine ya ukurutu ambao huenezwa kwa njia ya kugusana kati ya mnyama na mnyama (mwenye ugonjwa na asiyekuwa na ugonjwa). Huathiri wanyama kama ng'ombe, kondoo, nguruwe, mbwa, mbuzi, farasi.

## Dalili za ugonjwa wa ukurutu

- Mnyama ambaye tayari ana ugonjwa huu kujikuna sana na mara kwa mara na hii ni kutokana na muwasho unaokuwepo kwenye ngozi.
- Kutokana na kujikuna mara kwa mara, manyoya huanza kunyofoka siku hadi siku.
- Ngozi ya mnyama muathirika na ugonjwa huu huanza kutoa unga unga.
- Ngozi ya mnyama pia huwa ngumu na hukakamaa.
- Mnyama huwepa kupata vivimbe katika sehemu mbali mbali kama shingoni, kwenye mabega, mgongoni na hata usoni.
- Ngozi ya mnyama pia huweza kuvimba na huwasha sana na ndiko kunakopelekea kujikuna.

## Tiba

Mnyama aliye na ugonjwa huu huweza kutibiwa na kupona kabisa kwa kutumia aina mbili za dawa ambazo ni dawa za sindano au dawa za kuogesha.

## Dawa ya sindano

Mnyama atibiwe kwa kutumia dawa aina ya Ivermectin na kwa kuzingatia utaratibu kutoka kwa mtaalamu wa mifugo kwani kila mnyama hupewa dozi tofauti na mwingine.

## Dawa ya kuogesha

Dawa zinazotumika kwa ajili ya kuogeshea ni zile ambazo zina kiini tete kiitwacho Amitraz kama vile TIXFIX, BAMITRAZ na TWIGATRAZ.

## Namna ya kukinga ugonjwa wa ukurutu

- Kama mfugaji, hakikisha unafanya usafi wa banda mara kwa mara.
- Ogesha mifugo kila wakati kulingana na utaratibu unaotolewa na wataalamu wa mifugo.
- Pulizia banda la mifugo dawa zenye Amitraz ili kuua utitiri.
- Ikiwa umegundua kuna mnyama ameanza kuonyesha dalili za ugonjwa huu, mpatie tiba mapema ili kuwakinga wengine na ikiwezekana wapatie na wanyama wengine wote ambao bado hawaonyesha dalili hiyo.

# Matumizi sahihi ya mbolea ya samadi itokanayo na kinyesi cha Popo

***Ni ukweli usiopingika kuwa, wakulima wengi kwasasa wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mbolea kwa ajili ya kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao mbalimbali jambo ambalo huweza kutatuliwa kwa kutumia njia mbalimbali na matumizi sahihi ya mbolea za asili ikiwemo samadi itokanayo na kinyesi cha popo.***

**Festo Sikagonamo**

Popo hupatikana katika maeneo mbalimbali kama vile kwenye mapagala, miti, mapango au kwa kujenga banda na kuliegesha shambani kisha popo kuingia na kufanya makazi, na baadaye kutoa kinyesi chao ambacho baadaye mkulima anaweza kukusanya kwa ajili ya matumizi ya kilimo.

Cleophace Mwombeki toka Kijiji cha Vianzi [Morogoro] ni mtaalamu wa kutengeneza mbolea inayotokana na samadi ya popo ujuzi anaosema aliupata miaka kadhaa iliyopita baada ya kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mbolea kwa ajili ya mazao yake.



Kinyesi cha popo

## Jinsi ya kuandaa/kutengeneza

Kama ilivyo kwa mbolea zingine za asili zinazotumika katika uzalishaji wa mazao mbalimbali, kuna hatua ambazo ni lazima kuzifuata ili kuweza kupata mbolea bora na yenye tija kwa mkulima.

Ili kupata mbolea bora itokanayo na popo huna budi kufanya yafuatayo;

- Chukua samadi ya popo kiroba kimoja ambacho kitakuwa na ujazo wa kilogramu 25.
- Andaa chombo chenye ujazo wa maji kiasi cha lita 200 [yaani pipa].
- Chukua samadi uliyoweka kwenye kiroba kisha dumbukiza kwenye pipa lako.
- Mimina maji mpaka kwenye ujazo wa pipa lako.
- Funika mbolea hiyo kwa kitu ambacho hakiwezeshi hewa kutoka, lengo ni kulinda virutubisho vilivyomo kwenye mbolea.
- Acha kwa muda wa siku tatu ikiwa imefunikwa.
- Siku ya tatu funua na anza kuikoroga na utakuwa unafanya hivyo kila baada ya siku tatu, kufunua, kukoroga na kisha kufunika. Utafanya hivyo kwa muda wa siku 21

## Nini hufuata baada ya siku 21

Baada ya siku 21 andaa vyombo vya kuhifadhia mbolea yako vyenye ujazo wa lita 600 ujazo huo ni sawa na mapipa matatu.

Chukua maji lita 400 sawa na mapipa mawili, kisha changanya na mbolea hiyo iliyokuwa imeandaliwa kwa siku 21.

Lengo ni kutaka kupunguza nguvu iliyomo kwenye mbolea ili isije ikaleta madhara kwenye ardhi na kuunguza mazao pia.

Ikishachanganywa kwenye lita 400 na kukoroga vizuri mbolea yako itakuwa tayari kwa ajili kutumika shambani, na unaweza kuiweka kwenye vyombo vidogo vidogo ambavyo itakuwa ni rahisi kubeba wakati wa kupeleka mbolea shambani

## Jinsi ya kutumia

Kila mmea utaunywesha mbolea kwa kipimo cha robo ya kikombe kidogo cha chai na mbolea hii hutumika wakati mmea tayari umefikisha siku 21 yaani wiki tatu toka kuoteshwa.

Mbolea hii huweza kutumika kwa mazao ya aina mbalimbali yakiwemo ya mboga na matunda, mazao ya nafaka na mazao mengine yale ya muda mrefu (ya kudumu)

## Faida ya mbolea hii

Mwombeki anasema kuwa "tangu nilipoanza kuitumia mbolea hii nimepata mafanikio makubwa katika kuongeza tija ya uzalishaji, lakini si tu kwangu bali hata wakulima wenzangu ambao nimewafundisha wamekuwa wakitoa shuhuda za ufasini wa mbolea ya popo kwenye mazao yao''.



Mbole itokanayo na kinyesi cha popo

''Nimeweza kupunguza utegemezi wa mbolea, nimekuwa huru na ninaweza kuandaa mashamba yangu wakati wowote kwa kuwa sina changamoto tena ya mbolea na mbolea hii inaweza kudumu katika ardhi kwa takribani miaka kumi'' aliongeza.

Bw. Mwombeki anaeleza kuwa mbolea ya popo imekuwa msaada mkubwa sana kwake hasa wakati wa mabadiliko ya tabia nchi kwa kuwa inaweza kuufanya mmea na udongo ukawa na unyevu kwa muda mrefu na hivyo kusaidia mazao yasiathirike kirahisi.

''Kwa maeneo mengine mbolea ya popo imekuwa na soko kubwa sana na inahitajika kwa kiwango kikubwa mfano kwa Zanzibar kilogram moja ya bidhaa hii inauzwa sh. 1500" alisema

## Wito kwa serikali

''Naiomba serikali ijaribu kuunga mkono jitihada za wakulima wadogo ambao wanabuni teknolojia mbalimbali na rahisi za kilimo hasa pembejeo za asili'' alisema.

Bw. Mwombeki anasema kuwa, serikali kama itatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kufanya tafiti za mbolea za asili inaweza kumsaidia mkulima ambaye kila mwaka ana uhitaji mkubwa wa mbolea kwa ajili ya kuzalisha.

***Kwa maelezo zaidi kuhusiana na mbolea ya popo wasiliana na Bw. Mwombeki kwa simu namba 0768391947***

# Ni muhimu kuwa na mzani katika ufugaji wa nguruwe

***Katika ufugaji wa nguruwe, matumizi ya mizani kwa upimaji wa uzito ni nyenzo muhimu katika kujipima/ kujitathimini kama mfugaji yupo katika mstari sahihi kufikia malengo aliyojiwekea. Kwa hiyo matumizi ya mzani ni nyenzo muhimu ili kufanya ufugaji wenye tija***

**Flora Laanyuni**

## Faida za mizani na upimaji uzito wa nguruwe

Kujua uzito wa nguruwe hasa wakati wa kununua husaidia kufahamu thamani ya kile unacholipia fedha.

Katika zama hizi za teknolojia ni vigumu sana kwenda kuona nguruwe kabla ya kununua, sana sana utatumiwa picha au video tu. Hivyo ni muhimu ukafahamishwa uzito na umri wa nguruwe unayetaka kununua ili ujiridhishe kama anafikia kiwango unachotaka au la, na hivyo ufanye uamuzi sahihi wa kununua.

Baada ya kununua na kumfikisha shambani kwako, unaweza kujithibitishia (kama unao mzani) kuwa uzito wake ni sawa na ule ulioahidiwa. Hapo utajipatia nguruwe wa thamani halisi ya pesa uliyolipa.

Fahamu kwamba ukinunua nguruwe ambaye hajafikia kiwango Fulani, mfano, mtoto (weaner) wa wiki 12, awe na uzito wa kilo 35 – 40, chini ya hapo, utakuwa na kazi ya ziada na utaingia gharama kubwa kumlea (kama ni jike) ili afikishe walau kilo 120 wakati wa kupandwa, na inawezekana hata asifikishe uzito huo unaoshauriwa.

Hivyo wakati wa kununua, hata kama ni mbegu bora usipofuata viwango sahihi vya uzito, itakuwa hasara kwani hata nguruwe walioendelezwa wasipotunzwa vizuri, hawawezi kuleta matokeo tarajiwa iwe kwenye nguruwe wa nyama au wa mbegu.

Watoto wanapoachishwa kunyonya katika umri wa siku 20 hadi 35 uzito (weaning weight) unaoshauriwa ni walau kilo 7-8. Chini ya hapo unaweza kufanya maamuzi kadri ya viwango ulivyojiwekea, mfano, kama uzito ni chini ya kilo 6, kutoendelea nao kwa sababu watakusumbua na kugharimu sana kuwafuga ili wakue katika viwango vinavyotakiwa.

Majike wanaopandishwa mara ya kwanza, inashauriwa wawe na uzito usiopungua kilo 120. Hapo jike anakuwa amejengeka vizuri mfumo wake wa uzazi na mifupa na atakuletea matokeo mazuri katika maisha yake yote ya uzaaji hapo baadae lakini pia ataweza kuhimili kupandwa hata na dume mkubwa, yaani mwenye kilo 200 na zaidi.




*Moja wapo ya mzani ambao hutumika kupima uzito wa nguruwe*

Katika rika mbalimbali mara nyingi hatua mbalimbali za ukuaji wa nguruwe au ubadilishaji wa lishe yao, hutenganishwa kwa uzito. Mfano, weaner atakula starter mpaka afikishe uzito wa kilo 25. Baada ya hapo anakuwa grower mpaka atakapofikisha kilo 45, halafu anaingia kwenye hatua ya finisher mpaka kilo 95 hadi 105. Mizani itakuwezesha kupambanua hatua hizo mbali mbali na kuwapa lishe sahihi.

Unapofuga nguruwe wa nyama upimaji utakusaidia kuuza kwa tija na kadri ya malengo yako kama utapima uzito wa nyama baada ya kuchinja, badala ya kukadiria tu uzito. Nguruwe wa kisasa huwa na mwonekano wa umbo dogo, lakini ukimweka kwenye mzani utashangaa uzito mkubwa alio nao.

Wakati wa kutibu dawa zote hutolewa kwa kufuata uzito wa mnyama hivyo ukifahamu uzito wa nguruwe wako ni rahisi kuwapatia dozi na matibabu sahihi.

### Kupima chakula

Wakati wa kuchanganya chakula unahitaji kupima uzito wa makundi mbali mbali ya viinilishe (ingredients) ili utengeneze mlo kamili (balanced ration) kwa usahihi.

### Wakati wa kulisha

Tunaona, kwa mfano, jike anayenyonyesha inatakiwa alishwe kilo 2.5 hadi 3 kwa siku kwa ajili ya mwili wake, na kilo 0.4 kwa kila mtoto. Hivyo jike mwenye watoto 10 atalishwa jumla ya kilo 7. Hapa pia, mzani utafanikisha mahesabu yako.

### Kujiwekea malengo, viwango na tathmini

Ni muhimu kufanya tathmini katika mradi wako kwa kupima nguruwe kila baada ya muda fulani, labda kila baada ya wiki moja au mbili, ili kuona kama wanafikia malengo na viwango vyako. Kama hawafikii, utatafuta kujua sababu (kama ni lishe duni au matunzo kwa ujumla) na kurekebisha mapungufu mpaka ufikie viwango vyako na hatimaye kupata tija uliyokusudia.

***Kwa maelezo zaidi wasiliana na Abrogast Msangawale kwa simu namba 0785000777***

# Lishe bora husaidia ukuaji wa mtoto

***Kila familia na jamii inapaswa kufahamu nini huhusu lishe? Hii ni kwasababu karibu nusu ya vifo vya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kila mwaka hutokana na ukosefu wa lishe bora na ya kutosha, unaosababisha kudhoofika kwa kinga mwili na kushindwa kupambana na magonjwa.***

**Erica Rugabandana**

Endapo mama hakupata lishe ya kutosha wakati wa ujauzito au mtoto wake hakupata lishe ya kutosha ndani ya siku 1000 za mwanzo wa maisha yake, ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili pamoja na maendeleo yake hudumaa. Hali hiyo hairekebishiki pale mtoto atakapokuwa mkubwa, itamuathiri mtoto kwa kipindi chote cha maisha yake.

Utapiamlo hujitokeza pale mwili unapokosa kiasi cha kutosha cha nishati (kalori,protini, wanga, mafuta, vitamini, madini na lishe nyingine zinazohitajika kwa ajili ya kufanya viungo vya mwili vikue na kufanya kazi vizuri. Mtoto au mtu mzima anaweza kupata tatizo la utapiamlo kwa kukosa lishe ya kutosha au kupewa lishe zaidi ya inavyohitajika.



Ili mtoto awe na afya bora anahitaji kupata lishe bora tangu akiwa tumboni

***Kila familia na jamii ina wajibu wa kufahamu kuhusu lishe bora kwa mtoto***

1. Mtoto mdogo hana budi kukua na kuongezeka uzito kwa haraka. Tangu anapozaliwa, mtoto apimwe uzito mara kwa mara kutathmini ukuaji wake. Endapo upimaji wa mara kwa mara utaonyesha kuwa uzito wa mtoto hauongezeki, au endapo wazazi au walezi wengine watabaini kuwa mtoto hakui, hiyo ni ishara kuwa kuna tatizo. Itabidi mtoto apelekwe kwa mtaalamu wa afya.
2. Maziwa ya mama ndicho chakula na kinywaji pekee anachohitaji mtoto mchanga katika miezi sita ya mwanzo ya maisha yake. Baada ya miezi sita, mtoto anahitaji aina mbalimbali za vyakula sambamba na maziwa ya mama ili kuhakikisha kuwa anakua akiwa na afya na maendeleo mazuri.
3. Kuanzia umri wa miezi 6, kutokana na ongezeko la mahitaji ya nishati, mtoto anapaswa kula mara mbili hadi tatu kwa siku, kutoka miezi 9 hadi 23, anapaswa kula mara tatu hadi nne kwa siku huku akiendelea kunyonya. Kutegemeana na hamu ya mtoto ya kula, mtoto anaweza kupewa kiasi kidogo cha tunda au mkate uliopakwa siagi ya karanga wakati akisubiri muda wake wa chakula. Mtoto alishwe chakula kidogo kidogo na kuongeza aina na kiasi cha chakula kadiri atakavyokuwa akiendelea kukua.
4. Wakati wa kulisha mtoto ni wakati wa kujifunza, kujenga upendo na mawasiliano, mambo ambayo huchochea ukuaji wa mtoto kimwili, kijamii na kitabia pamoja na maendeleo yake. Wazazi au walezi wengine wanapaswa kuzungumza na watoto wakati wanapowalisha, aidha wawalishe watoto wa kike na wa kiume katika hali sawa na kwa upole bila kubagua.
5. Watoto wachanga na wale wadogo huhitaji vitamini A ya kutosha kwa ajili ya kuwasaidia katika kinga ya magonjwa, kuimarisha macho yao na kuwasaidia kukua. Vitamini A huweza kupatikana katika matunda na mbogamboga, mafuta mekundu ya mawese, mayai, bidhaa za maziwa, maini, samaki, nyama, vyakula vilivyoongezwa vitamin A pamoja na maziwa ya mama. Katika maeneo ambayo yana tatizo la vitamin A, matone ya vitamini A yanaweza kutolewa kwa watoto wa umri wa miezi 6 hadi miaka 5 kila baada ya miezi minne hadi sita.
6. Watoto huhitaji vyakula vyenye madini chuma kwa wingi ili kusaidia kulinda miili na akili zao pamoja na kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa upungufu wa damu (anemia). Vyanzo vikuu vya madini chuma ni vyakula vya aina ya nyama kama vile maini, minofu na samaki. Vyanzo vingine vizuri ni vyakula vilivyoongezwa madingi chuma na vidonge vya madini chuma.
7. Madini joto ni muhimu sana katika chakula cha mama mjamzito na mtoto kwa ajili ya maendeleo ya akili ya mtoto. Ni muhimu kuzuia tatizo la uwezo mdogo wa kujifunza na udumavu. Kutumia chumvi iliyoongezwa madini joto badala ya ile ya kawaida huwapatia mama wajawazito na watoto wao kiasi cha kutosha cha madini joto.
8. Kadiri mtoto anavyoongeza ulaji wa vyakula na unywaji wa vimiminika ndivyo anavyozidi kuwa katika hatari zaidi ya kupatwa na magonjwa ya kuharisha. Uchafu katika chakula ndicho chanzo kikubwa cha ugonjwa wa kuhara na magonjwa mengine ambayo husababisha watoto wapoteze viini lishe na nishati inayohitajika kwa ukuaji na maendeleo yao. Usafi, maji salama, utayarishaji na uhifadhi mzuri wa chakula ni mambo muhimu sana katika kuzuia magonjwa.
9. Wakati wa ugonjwa watoto huhitaji vimiminika zaidi pamoja na kulishwa chakula na kunyonyeshwa mara kwa mara. Mtoto akipona aongezewe chakula ili kufidia viinilishe na nishati iliyopotea kutokana na ugonjwa.
10. Watoto wembamba sana na/au waliovimba hasa uso na miguu huhitaji huduma maalumu ya tiba. Watoto wenye hali hii wapelekwe kwa wataalamu wa afya au hospitalini kwa ajili ya uchunguzi na tiba.

# Kilimo hai kimenifungua macho na kunionyesha fursa za kilimo

***"Mwanzoni ni kama nilikuwa gizani, sikuwa najishughulisha na kitu chochote Zaidi ya kukaa nyumbani, sikuwahi kujua kama nina nguvu na nikisimama kama mama bora naweza kuzalisha vitu mbalimbali kwa faida ya familia yangu, hakika mimi ni kipofu niliyeona"***

**Flora Laanyuni**

Ndivyo alivyoanza kueleza Bi. Renalda Lawrent, kutoka Kijiji cha Kambi ya simba (wilayani Karatu) ambaye kwasasa anajishughulisha na uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa misingi ya kilimo hai.

## Maisha kabla ya kilimo hai

Bi. Renalda anasema kuwa, hapo mwanzo mara baada ya kuolewa, hakuwa akifanya kazi yeyote zaidi ya kuwa mama wa nyumbani, na mara moja moja kushiriki katika kilimo hususani uzalishaji wa mahindi ambao ulikuwa ukifanywa kulingana na msimu wa mvu pekee.

Hata hivyo, mazao hayo mara baada ya kuvunwa ndiyo hutumika kwa ajili ya kulisha familia na kuuza sehemu kidogo kwa ajili ya kununua mahitaji mengine ya familia kama nguo.

Mama huyu mwenye familia ya watoto 6 anaongeza kuwa, haikuwa kazi rahisi kuitunza familia yake kwa kile kidogo wanachozalisha, lakini hakuwa na suluhu nini afanye na hivyo kuhisi kuwa hivyo ndivyo tu maisha yalivyo.

## Ilikuwaje mpaka kuanza kuzalisha kwa misingi ya kilimo hai

"Mwaka 2017, nilipata elimu ya ujasiriamali kupitia shirika la TRIAS walioweza kunifungua macho na kunifundisha wajibu wa mama katika familia, namna ya kuitumia nguvu yangu kwa faida lakini pia namna ya kuzalisha kwa wingi na kupata faida" alisema.

Bi.Renalda anaeleza kuwa, alipata mafunzo ya biogesi ambayo ina faida nyingi katika kilimohai na ni muhimu sana mkulima au mfugaji kuwa nayo nyumbani kwake.

## Maisha baada ya kupata elimu ya kilimo hai

Nilikuwa nafuga ng'ombe hivyo mara baada ya kufundishwa kuhusu biogesi





*Bi. Renalda alifurahia jarida la Mkulima Mbunifu (Nyuma ni masalia ya mabua mara baada ya kulisha mifugo ambayo baadaye hutengenezea mbolea ya mboji), angalia picha ndogo pembeni*

na kufungiwa mtambo nikaanza rasmi kutumia disemba 2017 na wakati huo huo nikaanza kuotesha migomba, maua, mbogamboga na kutengeneza shamba langu kwa mpangilio wa kilimo hai.

Baada ya miezi michache nilianza kuona faida ya kilimo hai kwani, biogesi yenyewe iliweza kunipatia moto ambao ulinipa uhuru na muda wa kutosha kuendeleza kilimohai kwani sikuwa na harakaharaka ya kukimbia kutafuta kuni hivyo nikaanza kufurahia kilimohai na kuweka juhudi sana shambani.

Hakuishia hapo tu, alianza kuzalisha mahindi yale yale katika shamba lilelile lakini kwa kutumia kilimo hai hivyo mavuno yakaongezeaka na chakula cha mifugo kikapatikana kwa wingi.

Niliweza pia kuona fursa, kwani mara baada ya kuanza kutumia bioslari katika migomba na katika shamba langu la mahindi, nilijiongeza kuanza kuzalisha malisho ya matete kwa ajili ya ng'ombe na kwa kutumia mbolea hiyo niliweza kupata malisho mengi ambayo nayakata mara kwa mara kulishia.

## Faida za kilimo hai

Bi. Renalda anaeleza kuwa toka aanze kuzalisha kwa misingi ya kilimo hai ameweza kupata faida mbalimbali kama ifuatavyo;

- Kuzalisha mazao mbalimbali kwa kutumia gharama nafuu kwani malighafi zinazotumika zinapatikana katika mazingira ya nyumbani.
- Kupata mavuno bora na mengi ya mahindi kuliko awali.
- Kuweza kuzalisha matunda yatokana na migomba kwa ajili ya familia yake.
- Kulibadilisha eneo la nyumbani toka kwenye ukame na kuwa kwenye ukijani ikiwa ni pamoja na kuweza kuotesha maua.
- Kupata fedha kwa kuuza mazao mbalimbali kama mahindi ya kula pamoja na mbegu, ndizi, maziwa na mbogamboga.
- Kupata moto wa uhakika masaa 24 bila kuhangaika na kupoteza muda kutafuta kuni lakini pia bila kuharibu misitu.
- Kupata mbolea inayotokana na wanyama pamoja na mabaki mbalimbali ya mimea toka shambani.
- Kushirika kwenye makongamano mbalimbali ya wakulima hivyo kupata fursa ya kujifunza Zaidi kwa wakulima wengine waliofanikiwa.
- Kuwa na uhakika wa chakula cha mifugo msimu wote wa mwaka kwa kuhifadhi malisho ya ziada pamoja na kuwa nae neo la kuzalisha malisho pekee.

## Vipi kuhusu Mkulima Mbunifu

"Jarida hili nilianza kuliona mwaka huu mwezi wa 10 katika maonyesho ya wakulima Karatu, na niliposoma nakala mbili tu niligundua kuwa lina manufaa kwangu kwani nimejifunza namna ya kupanua miradi yangu ya kilimo hasa kwa kufuga mbuzi na kuku lakini pia namna rahisi ya kuzalisha mbogamboga katika eneo dogo"alisema.

Bi. Renalda ameongeza kuwa, kupitia jarida hili ameona aina bora ya mbuzi na namna ya kufuga, na tayari ameshaanza kutafuta mbuzi hao ili aanze kufuga mapema mwaka 2022.

"Nimejifunza pia namna ya kuzalisha mbogamboga kwa kutumia mifuko hivyo naanza kukusanya mbolea kwa ajili ya uzalishaji. Nawashauri tu wakulima wengine wahakikishe wanapata nakala za jarida hili kwani kwa muda mfupi nimeona faida yake lukuki" aliongeza.



Haki zote zimehifadhiwa ©2022 *Mkulima Mbunifu*